*SWAHILI FORUM 27 (2020): viii-xii*

# MAPITIO

***Swahili Muslim Publics and Postcolonial Experience.*** **Kai Kresse. 2018. Bloomington: Indiana University Press. k. 237. SKU 9780253037541 & 2019. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota. k. 256. SKU: 987998708329911.**

Ningependa kusisitiza sifa chache tu miongoni mwa sifa nyingi za kitabu hiki kilichoandikwa na msomi Kai Kresse. Sifa hizo zinastahili kutiliwa mkazo na hakika ndizo zilizoifanya kazi hii kuwa mchango wenye thamani kubwa sana katika Taaluma za Kiswahili, Anthropolojia, Falsafa, Ubaadaukoloni na nyingi nyenginezo.

Kazi hii iliyochapishwa na Mkuki na Nyota mwaka wa 2019 imegawanyika katika sehemu mbili: sehemu ya kwanza “Conceptualizations” inajadili dhana na utaratibu wa kuunda dhana zinazotokea utafiti huu na zinazotumika katika kuchambua data alizozikusanya; ya pili “Readings” inamwongoza msomaji kwenye utaratibu wa kusoma matini, kuyaelewa na kuyafafanua ili kupaza sauti za hadhara zinazoibuka katika utafiti na kuzisikiliza kama zilivyo, yaani hadhara za Kiislamu za Waswahili na mazoea yao ya kiubaadaukoloni.

Anachokifanya Kai Kresse katika kazi yake ni kuchambua matini ya Kiswahili ya aina tatu: kwanza, kigazeti cha Kiislamu cha *Sahifa* kilichoandikwa na kutolewa na Sheikh Al-Amin bin Ali Mazrui (1891-1947) kwenye miaka ya thelathini, karne iliyopita; pili, gazeti la Kiislamu la *Sauti ya Haki* lililohaririwa na Sheikh Muhammad Kassim Mazrui (1912-1982) na kutolewa kwa mwongo mmoja kwanzia mwaka wa 1972; tatu, “Elimika na Stambuli”, kipindi kilichotangazwa na idhaa ya Kiislamu ya *Radio Rahma* kwanzia mwaka wa 2005 mpaka 2007.

Ni muhimu kufafanua kuwa uchambuzi wake hauhusu matini kwa maana ya maandishi tu, bali matini ya kianthropolojia kama Karin Barber anavyoyafafanua, yaani maandishi pamoja na njia na vitendo vya wanajamii vya kuwasiliana na kujadiliana (Barber 2007). Kresse anakusanya yale yanayosimuliwa katika vyombo tofautitofauti vilivyoumba hadhara maalum katika muktadha wa Mombasa (na wa dunia, kwa upana zaidi, anavyosisitiza Profesa Hamza Njozi, 2019). Na ndivyo anavyojiwezesha kuzilinganisha hadhara hizo na kufafanua mitagusano na tofauti baina yao, kwa kuelezea vipengele vinavyojitokeza na kuzithamini, na kutafakari juu ya ujuzi unaozalishwa kutokana na hadhara hizo, ujuzi wa kijamii, ujuzi unaotokea kwa namna jamii inavyofahamika na kuumbika na wanajamii wake kujiunda. Ndiyo sababu ya kuchanganua matini kwa undani na kusikiliza kwa makini sauti zinazozungumza kwa kuyapitia. Uangalifu huo unazihusu hadhara zenye historia, falsafa, siasa, jamii, utamaduni, na dini yao yenyewe, pamoja na mahusiano na mitagusano hizo hadhara zinayoundwa nayo. Uangalifu huohuo unatusaidia kufumbua macho na kuwa watamazaji na kusikiliza kwa makini kama wasikilizaji wanaojihusisha na matini huku wakielewa na kufurahia ujuzi ambao, mwishowe, unachukuliwa ipasavyo, yaani ujuzi ulio na umuhimu sawa na ujuzi unaotokea kokote kwengineko.

REVIEW

Kresse anataja na kujadili aina mbalimbali za hadhara. Hadhara zinaundwa na kuumbwa kwa kupitia masimulizi, majadiliano, mawasiliano ya washiriki wanaojihusisha, yaani wale wote wanaohudhuria, kujiunga na kuchangia kwenye hadhara hizo. Tukizingatia siasa na vile vinavyoitwa 'vitendo vya kisiasa' swala maalum linaibuka mara kwa mara: ni nini kinaweza kuchukuliwa haswa kama vitendo vya kisiasa? Tuvielezee vipi vitendo vya aina hiyo? Tukilinganisha kinachotokezea kwenye intaneti, mtandaoni (*online*), na yale yanayotokezea kwenye maisha yaliyo nje ya mtandao (*offline*), wasomi wengi wanakataa kuyathamini yale yanayojadiliwa mtandaoni badala yake wanayathamini zaidi yaliyo nje ya mtandao (*offline*). Hoja mojawapo wanayoitoa ni kwamba uanaharakati wa kisiasa hautendeki mtandaoni bali unahitaji kutendeka nje ya mtandao. Watu wanapaswa kushiriki kwenye vitendo maishani mwa nje ya mtandao ili kuyafikia malengo yao na kuyabadilisha yale yanayowezekana kubadilika. Hata hivyo, hadhara si inaundwa na kuumbwa kupitia masimulizi na majadiliano ya wanaoshiriki? Si kwamba majadiliano, licha ya chombo yanachokipitia, ndiyo yanayoumba hadhara kama msomi Michael Warner (2002) anavyoelezea? Si kuna matokeo maalum na uwezeshaji maalum unaosababishwa na majadiliano hayo haswa kwa kupitia majadiliano yenyewe?

Tunachozungumzia hapo nadhani ni uwezo wa kuathiri masimulizi na majadiliano yalio nao, na vilevile uwezo wa kuathiri wa chombo kinachotumika. Sheikh al-Amin bin Ali Mazrui aliwezesha uumbaji wa hadhara kutokana na nafasi yake maalum katika jamii yake, pamoja na kuwa kadhi, kwa hivyo kuwemo kwake katika mfumo wa utawala wa kikoloni (kama anavyosisitiza Bwana Kresse huku akionyesha nafasi kinzani ya Sheikh al-Amin kwenye jamii yake mwenyewe), na kigazeti cha *Sahifa* kilikuwa kinawakilisha na kusimulia maoni yake. Hata hivyo, tukitazama njia yenyewe ya mawasiliano katika muktadha wake (yaani uwezo wake wa kuathiri muktadha uliopo) na tukikubali kuwa kigazeti kilisomwa na kupewa nguvu mikononi mwa watu wengi walio pengine washiriki wa mabaraza mbalimbali, basi hadhara iliyoumbwa ni pana zaidi kuliko tunavyoweza kufikiria.

Kigazeti cha *Sahifa* hakikuwa jukwaa la Sheikh al-Amin la kusambaza maoni yake tu, bali kilikuwa chanzo cha kuanzisha na kuzalisha hadhara yenyewe. Na hayo yanadhihirika vilevile tukichunguza kwa undani, kama Kresse alivyotufafanulia, mtindo wake wa kuandika, balagha aliyoitumia na ufasaha aliofaidika nao. Sheikh al-Amin alikuwa anakitumia kiima *sisi* kuwaelekeza wasomaji wake, na ni katika kitendo chake hicho cha kujitafutia na kujipatia nafasi kwenye jamii (*self-positioning*) pamoja na kutafutiwa na kupatiwa na jamii nafasi hiyohiyo (yaani kuwa *self-positioned*) kwamba hadhara inakuwa pana zaidi, kwamba mwenyewe aliwafungulia mlango wale wote watakaoendelea kujadiliana na kushauriana, hata kama si kupitia chombo hichohicho.

Kitendo hicho kinaelezewa vizuri sana vile Kresse anavyotufafanulia kipengele cha isimujamii, yaani matumizi ya mnyambuiliko *-an-* katika vitenzi mbalimbali – kama vile *kushauriana, kusaidiana, kukanyana* – kusisitiza kuwa kila kitendo ni cha mtu binafsi (kwa vile anajitafutia na kujipatia nafasi katika jamii) na kuwa cha watu wote kwenye hadhara (kwa kuwa anatafutiwa na

kupewa nafasi). Kwa hivyo, Kresse anapotaka kutuelezea uumbaji na uzalishwaji wa ujuzi, ambao ndio ujuzi wa Kiislamu wa Waswahili, anatufafanulia namna ujuzi unavyozaliwa kwenye uwiano baina ya kitendo cha mtu binafsi na vitendo vya wenzake. Anatuelezea namna dhana ya "nafasi inayotokea kwa mtu binafsi"[1] (pahala mtu alipo wakati uliopo na fursa inayoweza kumjia) na inayobeba kumbukumbu za jinsi alivyokuwa zamani, ni msingi wa fikra yake ya wakati uliopita endelevu (*past present continuous*). Anavyosema kwenye hitimisho la kazi hiyo, ndio uhusiano baina ya wakati uliopo (*present*) na hali ya kuwepo (*presence*) unaounda fikra ya wakati uliopita endelevu, yaani nafasi iliyomwezesha kufafanua umuhimu wa matini kwenye muktadha wa ubaadaukoloni, yaani baada ya ukoloni, kwa kupitia hadhara anazozizingatia. Dhana hiyo inasisitiza kuwa wakati uliopo unabeba kumbukumbu za wakati uliopita kuelekea na kutuelekeza katika wakati ujao: katika wakati uliopo kuna kiini cha wakati uliopita na cha mustakabali, Kresse anatukumbusha hilo akimnukuu msomi Achille Mbembe:

> "the present *as experience of a time* is precisely that moment when different forms of absence become mixed together: absence of those presences that are no longer so and that one remembers (the past), and absence of those others that are yet to come and are anticipated (the future)" (Mbembe 2001: 16 katika Kresse 2018: 197)

Huo ndio msingi wa ubaadaukoloni, yaani mazoea ya maisha ya kila siku wakati wa baada ya ukoloni, yaliyoathirika na ukatili wa kikoloni kwa namna mbalimbali, ila bila kusimamishwa nao, bali yanayoelekeza mustakabali (siku zijazo) wakati wote, kwa kuwa wanajamii wana uwezo wa kutumia vitendo vya kuyaathiri vilevile.

Kigazeti cha *Sahifa*, pamoja na gazeti la *Sauti ya Haki*, na kipindi cha redio cha "Elimika na Stambuli" ndizo hadhara tofauti ambazo si lazima zilinganishwe kwa ajili ya kuzihukumu tujue ni ipi bora au yenye faida zaidi, bali zote zina thamani za kuwa zimewawezesha washiriki wao kutafakari kwa njia mbalimbali juu ya nafsi yao na nafasi yao, tena kwa tabia ya kutaka kuyatenda na kuyaathiri maisha yao wenyewe. Kai Kresse anatambua mwenyewe kuhusu swala hili, anapohitimisha akisema kuwa ni lazima tusisahau kuwa mtindo wa kuandika wa Sheikh al-Amin bin Ali Mazrui unakumbusha mtindo wa kusimulia: msingi wake umekitwa katika jamii ambazo zina uzoefu wa *kujibizana*, *kushindana* au *kujadiliana barazani* (*na uani*). Aidha, tusiposahau kwamba maoni yake yalikuwa yanapingwa na baadhi ya watu wakati ule, hapo ndipo hadhara inapodhihirika zaidi, hata kama hadhara hiyo, au hizo, zilikuwa hazipitii chombo hichohicho cha kigazeti cha *Sahifa*.

Ndivyo mmaizi Michael Warner anavyofafanua hadhara, yaani nafasi inayoundwa na kuumbika kutokana na mawasiliano baina ya wanajamii walio na lengo moja (Warner 2002). Ndivyo alivyotuwezesha kuitambua hadhara pinzani pia, badala ya kuifikiria hadhara kama nafasi iliyoko kati ya serikali na wanajamii kwa lengo la kupatanisha maslahi yao, kama Habermas alivyoturithisha kutokana na mfumo wa nadharia za kimagharibi (Habermas *na wenzake* 1974).

[1] Mhojiwa mmojwapo kwenye muktadha wa utafiti wangu juu ya dhana ya 'nafasi' kwa vile inavyofahamika na kuundwa kupitia vitendo vya maisha ya kila siku ya vijana wanaojulikana kwa jina la *mapapasi*. Zanzibar Town, Unguja, 2019.

Kwa hiyo, ninamuunga mkono Profesa Hyder anaposifia mradi wa *Radio Rahma* na matukio yake (k. 180-184), na vilevile ninataka nisisitize hoja kuwa hadhara yoyote ile inayozalishwa na kuwawezesha wanaoiunda wenyewe ndiyo inayopaswa kusifiwa.

Kuna kipengele chengine ambacho ningependa kukigusia. Kila hadhara inazalisha ujuzi maalum na hadhara zinazochorwa katika kazi hiyo zinazalisha ujuzi maalum pia. Kazi hii ni mfano wa hali ya juu kabisa wa unyenyekevu ambao mmaizi anapaswa kuwa nao kila anapoanza kufanyia kazi mada au muktadha fulani. Sifa hiyo ndiyo inayowezesha kuweka pembezoni nadharia na dhana zilizotawala kwa kipindi kirefu sana katika taaluma za kijamii (na taaluma kwa jumla), yaani nadharia ya kimagharibi. Sifa hiyo ndiyo inayowezesha kufikiria upya dunia kwa kutumia mtazamo mbadala kama anavyopendekeza msomi Chakrabarty (2007). Kresse amefanikiwa kufikia lengo hili: kwanza kwa kushirikiana na kuyatafasiri matini aliyofanyia kazi (na hapo sifikirii kazi hii tu, bali ninarejelea kitabu cha *Guidance (Uwongozi)* pia, kazi ya Sheikh al-Amin Mazrui Kresse aliyoitafasiri na kuihariri pamoja na Profesa Hassan Mwakimako mnamo 2016); pili kwa kuchanganua matini istilahi mojamoja, yaani kwa kukaribia matini kwa uangalifu na usikilivu ili kutufafanulia ujuzi unaotokea muktadha alioufanyia kazi, kwa kutujulisha na kutufahamisha juu ya mitazamo ya kinadharia na dhana zinazoibuka hadharani, zinazoumbwa kwa kupitia mawasiliano na majadiliano.

Hakuna kinachobuniwa upya na mtafiti. Yote tayari yamo katika matini; changamoto kubwa ni kuyaona, kuyagundua, na kuyatatfsiri yafahamike na hadhara mbalimbali. Hiyo ndiyo sifa nyingine kubwa ya kazi hiyo, maanake kusomea ujuzi unavyozalishwa na kusambazwa, kuelewa maana yake kwa jamii iliyouzalisha pamoja na kuutafsiria ili uwe unapatikana kwa watu wengine wengi. Hii ndiyo changamoto na kazi ngumu. Kwa swala hili pia, kama kazi yake inavyoonyesha, Kai Kresse anafuata ushauri wa Chakrabarty (2007) kuwa tusiendelee kuchukua mfumo wa kinadharia wa kimagharibi kama mfumo pekee, bali tuuchukue ulivyo, yaani mfumo mmojawapo miongoni mwa mifumo mingine mingi inayotokea sehemu mbalimbali duniani. Na tukitaka kweli kufahamu jamii ya kibinadamu kwa jumla, basi hatuna budi kuelekeza bidii zetu kwengineko. Kwa kupitia kazi hii, Kresse ametutunukia mfano mzuri wa utafiti na ufafanuzi wa hali ya juu yaani kazi yenye "umakini na ufasaha mkubwa" kama anavyosisitza Profesa Hamza Njozi (2019).

Umuhimu wa kukaribia muktadha kwa mtazamo huo unamwezesha mtafiti kugundua na kufafanulia dhana mbadala zinazojitokeza katika muktadha wenyewe, ambao ndio mpana kuliko muktadha matini yanapozalishwa. Ujuzi unaumbwa kwa njia mbalimbali, tukichukua dhana ya matini yanayobadili na kubadilishwa, kama Kai Kresse alivyofanya. Masuala mengine yanafafanuliwa machoni mwetu. Kuhama kutoka katika nadharia tawala na kuhamia nadharia mbadala kunatajirisha ujuzi wetu wa jamii ya jumla. Chakrabarty alitoa wito, na Kresse ameitikia wito huo wa kuthamini nadharia zinazotokea kila pembe ya dunia.

*Irene Brunotti*

## Marejeleo

Barber, Karin. 2007. *The Anthropology of Texts, Persons and Publics: Oral and Written Culture in Africa and Beyond*. Cambridge: Cambridge University Press.

Chakrabarty, Dipesh. 2007. *Provincializing Europe: Postcolonial Thought and Historical Differene*. Princeton, NJ: Princeton University Press.

Habermas, Jürgen, Sara Lennox & Frank Lennox. 1974. The Public Sphere: An Encyclopedia Article (1964). *New German Critique* 3: 49-55.

Kresse, Kai (ed.). 2017. *Guidance (Uwongozi) by Sheikh Al-Amin Bin Mazrui: Selections from the First Swahili Islamic Newspaper*. Translated by Kai Kresse and Hassan Mwakimako. Swahili-English edition. Leiden: Brill.

Mbembe, Achille. 2001. *On the Postcolony*. Berkeley: University of California Press.

Njozi, Hamza. 2019. Mchango kwa ajili ya uzinduzi wa kitabu hiki kwenye Baraza la Kiswahili la Berlini, Taasisi ya Mashariki ya Kisasa / Chuo Kikuu cha Humboldt, Berlin, na Kongamano la Kimataifa la Kiswahili la 32, Chuo Kikuu cha Bayreuth, tarehe 20 Mei & 1 Juni 2019. Kimerekodiwa tarehe 18 Mei 2019, Morogoro.

Warner, Michael. 2002. *Publics and Counterpublics.* Brooklyn, NY: Zone Books.